JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI

Simu +255 784 / 767- 413 494
E-mail: muhezahighschool@gmail.com
Kumb Na. MHS / 21 /…….. /20……

MUHEZA HIGH SCHOOL,
S.L.P 420,
MUHEZA.

Tarehe: 20/ 05 / 2021

KWA:-

MZAZI / MLEZI WA MWANAFUNZI ……, S. L. P……, ……

YAH:MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MUHEZA HIGH SCHOOL HALMASHAURI YA WILAYA MUHEZA MKOA WA TANGA - KIDATO CHA TANO KWA MWAKA 2021/2022

1:0.Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha V katika shule hii kwa mwaka 2020/2021 ,tahasusi ya ……..Shule ipo umbali wa km 3.5 mashariki mwa mji mkuu wa Wilaya ya Muheza kuelekea Tanga Mjini.Kutoka kituo cha basi kikubwa cha Mji wa Muheza, usafiri waTax mpaka Muheza high School ni shilingi 4,000/=.Anatakiwa kuripoti shuleni ifikapo tarehe **…../ 07 / 2021, muhula wa masomo utakapoanza na mwisho wa kuripoti ni …. / 07 / 2021.**

2:0. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

2:1. Sare ya shule.

(a) Sare ya shule hii kwa wavulana ni mashati 2 light blue (Bluu Bahari) ya mikono mirefu yasiyobana na suruali 2 dark blue zenye mifuko 2 mbele na 1 nyuma isiyo ya kubandika, iwe ndefu ya kugusa kiatu, **isipungue upana wa chini inchi 16 chini** na mkanda wa suruari mweusi wa ngozi. Kwa wasichana ni mashati 2 light blue (BluuBahari) ya mikono mirefu yasiyobana na sketi 2 dark blue ndefu mpaka karibu na viatu zenye marinda ya kupanga na isiyobana; Kwa wanaovaa Hijabu, rangi ya hijabu ifanane na sare ya shule (Hijabu light blue-Bluu Bahari) bila urembo wa aina yoyote na sketi 2 dark blue ndefu mpaka karibu na viatu zenye marinda ya kupanga na isiyobana.

(b)Shamba dress:wavulana suruali nyeusi na fulana (form 6) ya blue isiyo na michilizi au maandishi yoyote. Wasichana gauni la dark green refu mpaka kwenye kiatu na lenye marinda ya kupanga na wanaotumia hijabu ni rangi moja na gauni.

(c)Viatu ni vyeusi vya ngozi vya kamba vya kufunika jozi mbili. Na soksi nyeusi angalau jozi 2.

(d)Sare ya shule kwa michezo ni **track suit** mbili dark blue kwa wavulana na kwa wasichana ni dark green. Na raba za michezo nyeupe kwa wote.

(e) Sweta la Dark blue lenye nembo ya shule. (Aje na 14,000/= atapatiwa hapa hapa shuleni)

Angalizo:*Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani Zaidi ya zilizotajwa hapo juu.*

2;2. Ada na michango ya shule:-

(a)Ada yashule.

Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000/= au 35,000/= kwa muhula mmoja kwa mwanafunzi wa bweni. Mwaka mmoja wa masomo una mihula miwili.

(b)Michango apasayo kulipa kila mwanafunzi anaporipot ishuleni ni:-

(i) Shilingi 5,000/= kwa ajili ya tahadhari.
(ii) Shilingi 2,000/= zabeji (nembo)yashule.
(iii) Shilingi 7,000/= kitambulisho na picha
(iv) Shilingi 10,000/= kwa ajili ya matibabu au 5,000/=kama ana bima ya afya.
(v) Shilingi 30,000/= zakulipa Ulinzi / Upishi.
(vi) Shilingi10,000/= za T-shirt moja yenye nembo ya shule.
(vii)Shilingi 30,000/= za taaaluma.
(viii) Shilingi 30,000/= Ukarabati
(ix) Shilingi 20,000/= mitihani ya kujipima.
(x) **Rim moja (A4) – Aje nayo shuleni.**

Jumla ya ada ya **muhula mmoja na michango** ni Shilingi**179,000/=** tunashauri ingiza kwenye akaunti ya shule **ya Muheza High schoo l NMB Ac. Na. 41901100027** kwa usalama wa fedha husika. **Ajena slip halisi yenye jina la mwanafunzi husika ya benki ya NMB aliyolipia Ada na Michango tajwa hapo juu. *HATUPOKEI FEDHA TASLIMU*.**

2:3. **Vifaa vya kujanavyo Shuleni:-**

(i) Kila mwanafunzi anatakiwa awe na **Dissecting kit** moja (Au aje na 30,000/= anunulie hapa shuleni).
(ii) Madaftari yaani **counter books (4 - Quires) zisizopungua saba (7)**, **anaweza kununulia shuleni.**
(iii) **Madaftari ya mazoezi 6 akiweza na fold files tano (5) kwaajili ya kutunzia test na mitihani yake.**
(iv) Godoro 1 (futi 3 kwa 6) na Chandarua (**Neti) kwa ajili ya kujikinga na Mbu** nyeupe/blue.
(v) Mto na foronya rangi ya pinki.
(vi) Shuka 2 za pinki.
(vii) Branketi jeusi au kijivu
(viii) Kijiko, kikombe bakuli na sahani.
(ix) Ndoo kubwa mbili za plastiki na **Calculator(Scientific Calculator) ni muhimu sana mwanao ajenayo.**
(x) Shule ni mahali pa kusoma na si kuonyesha mavazi.Nguo za nyumbani hazihitajiki shuleni hivyo **sanduku kubwa halitakiwi.**
(xi) Sanduku la bati lisilozidi upana wa 35cm na urefu wa 70cm. **Lisizidi vipimo hivi.**
(xii) School bag (mfuko wa kubebea madaftari) mweusi wa heshima.
(xiii) **Shule ina vitabu vya masomo mbalimbali ila havitoshelezi kwa kila Mwanafunzi, Ni vizuri akanunua vitabu vyake binafsi baada ya kupata ushauri hapa shule juu ya vitabu vifaavyo.**

*** **Ni muhimu mwanafunzi aje na "statement of results / result slip" na nakala yake moja ya matokeo yake kidato cha nne(Itolewayo na baraza la Mitihani la Tanzania).**

2:4. Vifaa vya usafi:- Jembe na mpini wake., Kwanja, Mfagio wa Ndani na nje, soft bloom

3:0. **Sheria na kanuni za shule hii.**

3:1. Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inanzingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Aidha unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo ufafanuzi wake zaidi utaupata ukifika shuleni.

(a) Heshimu viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wenzako na jamii kwa ujumla.
(b) Mahudhurio kamilifu katika kila shughuli ndani na nje upewayo na uongozi wa shule ni muhimu.
(c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni(Preparation) na kufauru mitihani kiwango cha daraja **I - III**
(d) Kuwahi kwa wakati uliyopangwa katika kila shughuli za shule na zingine utakazopangiwa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia maelekezo / Sheria juu ya kuwepo ndani au nje ya mipaka ya Shule.
(f) Kutunza usafi wa mwili pamoja na kutofuga ndevu/ usukaji nywele uliokubalika na kutunza mazingira ya shule.
(g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
(h) Kuvaa sare ya shule wakati wote wa vipindi darasani au ukiruhusiwa kutoka nje ya shule.

3:2. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa Shule mara moja.

(a) Wizi wa aina yoyote.
(b) Uasherati, uzinzi na ushoga
(c) Ubakaji
(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya au uvutaji wa sigara au bangi au kukutwa kwenye majumba ya starehe.
(e) Kupigana au kupiga au kufanya jaribio lolote la kujiua/kuua au kutishia kujiua/kuua.
(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
(g) Kudharau wimbo au Bendera ya Taifa.
(h) Kuoa au kuolewa au kuwekwa kinyumba.
(i) Kupata au kusababisha mimba au kuharibu(kutoa)mimba ndani au nje ya shule au kushiriki katika matendo hayo.
(j) Kugoma, kuchochea, au kuongoza uvurugaji wa amani na usalama wa shule au wanajamii.
(k) Kukataa adhabu uliyopewa na uongozi wa Shule.**Shule hii si mahali pa malumbano ya kidini au kisiasa.**
(l) Ni **marufuku** mwanafunzi kukutwa akimiliki au kuwa na **simu ya mkononi** muda wowote akiwa mwanafunzi hapa shuleni.

4:0. Mambo mengine muhimu.

(a) Medical examination form ijazwe na Mganga Mkuu wa hospitari ya serikali na kurudishwa shuleni.
(b) Fomu ya maelezo binafsi ya mwanafunzi na mzazi/mlezi kukiri kukubaliana na maelezo nasheria za shule irudishwe shuleni mwanafunzi anaporipoti.

5:0. **Tafadhari soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

……..

A.R. BIRUMO
MKUU WA SHULE

Jina la mwanafunzi----------

S.L.P----------

Tarehe----------

MKUU WA SHULE,
MUHEZA HIGH SCHOOL,
S.L.P . 420,
MUHEZA.

YAH; **UCHAGUZI WA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO 20…./20…..**

1. Ahsante sana kwa barua yako yenye kumb.MHS/23/----------/20------- tarehe --- ----/-------/20-------
ya kunijulisha kuwa nimechaguliwa kujiunga na kidato cha tano shuleni hapo.

2. Ninatoa ahadi kutii sheria zote za shule ambazo nimezisoma na kuzielewa.

3. Ninakubali / sikubali nafasi hii niliyopewa na Taifa.

4. Niko tayari kutimiza maagizo yote niliyopewa ya kujiunga na shule hii.

5. Historia fupi ya mwanafunzi husika.

PICHA YA MWANAFUNZI

Jina kamili ulioandikishwa shuleni	Shule ya msingi na sekondari ulizopitia	Tarehe ya kuzaliwa	Mahali ulipozaliwa	Dini /Dhehebu lako	URAIA
	MSINGI:				
	SEKONDARI:				

Nakiri kuwa maelekezo yote niliyotoa hapo juu ni sahihi.

6.0 Jina kamili la mwanafunzi…….sahihi…….... terehe……../…..20…..

==========

7.0 **Sehemu ya mzazi/mlezi kukubali kuchaguliwa kwa mwanafunzi husika.**

PICHA YA MZAI/MLEZI

7.1 Jina la mzazi/mlezi:…….Kazi: …….

Kata mzazi anapoishi…… kijiji / mtaa……wilaya……..

Namba ya simu ya mzazi / mlezi : ……S.L.P. ……,……..
Nakiri kuwa huyu ni mwanangu. Nakubali /Sikubali na fasi hii aliyopewa ya kujiunga na shule hii. Nakubaliana / Sikubaliani na sheria na maagizo yote ya shule aliyopewa ya kujiunga na shule hii. Naahidi kumuhudumia mwanangu kikamilifu na kushirikiana na uongozi wa shule katika kufanikisha maendeleo ya elimu yake.

Sahihi ya mzazi/mlezi……Tarehe:……/……20……
FUTA ISIYO HUSIKA

MUHEZA HIGH SCHOOL
P. O. BOX 420,
MUHEZA
DATE:……../…../20…..

KUMB No.: MHS / 21 / MED. ……./20……

SPECIAL REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

TO THE MEDICAL OFFICER

Name of student ----------
Form ---------- Term ---------- Year ----------

Dear Doctor

Please kindly examine the above named student to prove his/her fitness undertaking studies at our school.

1. X-ray ( ) 2. Urine ( ) 3. Stool ( )
4. Physical fitness ( ) 5. V.D ( ) 6. Tuberculosis ( )

A: (I) PRELIMINARY INFORMATION (BY THE STUDENT BEFORE THE DOCTOR)

NO	DISEASE	YES/NO	NO	DISEASE	YES/NO
1	Tuberculosis		10	Epilepsy	
2	Pneumonia		11	Ear, Nose and threat	
3	Asthma		12	Skin disorder disease	
4	Heart trouble		13	Anemia	
5	Recurrent indigestion		14	Operations	
6	Jaundice		15	Serious Accident	
7	Dysentery		16	Malaria	
8	Kidney and urinary trouble		17	Stomach trouble	
9	Nervous breakdown		18	Eye disorder	

(II) VACCINATIONS AND INNOVULATIONS HISOTRY

DISEASE	1ST DATE	2ND DATE	3RD DATE
Small pox			
Whooping cough			
Measles			
Yellow fever			
Cholera			

Official

B: MEDICAL EXAMINATION REPORT

(a) Weight

(b) Heat Beat

(c) Vision etc

MEDICAL CERTIFICATE

I have examined the above and consider that he/she is physically fit/unfit to undergo studies.

DOCTOR'S NAME & SIGNATURE ----------

DATE ----------